


# UQAB
Jarida la

*Toleo 16 - Shaaban 1439 AH / May 2018 Miladi*


# Miaka 97




# ya Kuomboleza na Kutaabika Chini ya Idhilali ya Ukoloni wa Urasilimali

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

حزب التحرير HIZB UT TAHRIR

KUMB: 08/1439 H Ijumaa, 26 Rajab1439 H 13/04/2018 M

# Hizb ut-Tahrir Kenya Yakumbusha Ummah kwa tukio la Huzni la kuangushwa Kwa Khilafah

**Taarifa kwa Vyombo vya Habari**

Ijumaa tarehe 13 April 2018, Hizb ut-Tahrir Kenya iliongoza Ummah kwenye ukumbusho wa tukio kubwa lililoacha Ummah wa Kiislamu kuwa yatima asokuwa na mlezi nalo ni kuvunjwa kwa Khilafah yapata miaka 97 sasa. Ukumbusho huu ulifanywa katika maandamano baridi baada ya swala ya Ijumaa katika Miji ya Nairobi, Mombasa, Kwale na Kilifi. Kauli mbiu kwenye maandamano hayo ilikuwa: **MuokoeniJanat_OkoeniGhouta_ SimamisheniKhilafah**

Katika maandamano hayo, Hizb imewakumbusha Waislamu kuwa uadui wa serikali ya Urusi dhidi ya walinganizi wa Khilafah sio mgeni kwani ilishirikiana pamoja na Uingereza katika kuiangusha Khilafah mwaka 1924. Kuangushwa kwake ndio chanzo cha madhila na masaibu yanayowakumba Waislamu kote duniani kwani Ummah ilipoteza ngao yake halisi; Khalifah aliyesifiwa na Mtume Muhammad (saw):(إنما الإمام جنة يقاتل من ورائه ويتقى به)
**Hakika ya Kiongozi ni ngao watu hupigana nyuma yake na kwake hupata hifadhi.**
[Muslim]

Maandamano haya yalikuwa sehemu tu katika ya kampeni ya kiulimwengu iliyoanzishwa na Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut-Tahrir ndani ya mwezi huu mtukufu wa Rajab. Kampeni hii imelenga kukumbusha na kuwataka Waislamu wachangamke katika kutekeleza faradhi miongoni mwa faradhi kubwa bali mama wa faradhi zote nayo kuisimamisha tena Khilafah. Ukumbusho huu unakuja ikiwa bado Waislamu wapo kwenye minyororo ya wakoloni makafiri ambao wanaeneza ufisadi katika ardhi na kuuwa mimea na wanyama .Basi huu ni ukumbusho utakao wafaa wenye kukumbushwa nao wataelewa kuwa kusimamisha Khilafah ndio suluhisho la kweli litakalo tatua matatizo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Na bila shaka siku ya kusimama kwake ndio Waumini watafurahi kwa nusra ya Mwenyezi Mungu (swt).

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut Tahrir Kenya**

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya**

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

حزب التحرير
HIZB UT TAHRIR

KUMB: 07/1439 H | Ijumapili, 21 Rajab 1439 H | 08/04/2018 M

# Tangazo la Kifo cha mmoja ya walinganizi wa Kiislamu Kenya

## Taarifa kwa Vyombo vya Habari

لَنَبْلُوَنَّكُمْ بِشَيْءٍ مِنَ الْخَوْفِ وَالْجُوعِ وَنَقْصٍ مِنَ الْأَمْوَالِ وَالْأَنْفُسِ وَالثَّمَرَاتِ وَبَشِّرِ الصَّابِرِينَ * الَّذِينَ إِذَا أَصَابَتْهُمْ مُصِيبَةٌ قَالُوا إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ

**Na Tutakutien katika misukosuko wa (baadhi ya mambo haya) hofu , njaa na upungufu wa mali na wa watu na wa matunda. Na wapashe habari njema wanaosubiri . Ambao uwapatapo msiba husema: 'Hakika sisi ni wa MwenyeziMungu, na Kwake Yeye tutarejea** [Al-Baqara: 155-156]

Kwa nyoyo zenye kuamini Qadhaa ya MwenyeziMungu na Qadar yake harakati ya Kiislamu ya Hizb ut-Tahrir Kenya, inawatangazia umma wa Kiislamu wote kwa ujumla na hasa Waislamu nchini kenya kifo cha

**Abdallah Ismail (**Mola Amrehemu**)**

Ndugu yetu Mola amrehemu, alikuwa mmoja wa wanachama shupavu wa Hizb ut-Tahrir akibeba ulinganizi wa haki wa kuregesha maisha ya Kiislamu kupitia kuisimamisha tena Khilafah kwa manhaj ya Mtume (saw); na wala hatumsifii MwenyeziMungu yoyote yule. Alipatwa na mauti Ijumaa asubuhi tarehe 6 Aprili, 2018 sawa na 19 Rajab 1439H baada ya kuugua kwa muda mfupi.

Kwa hakika wanaume wa kikweli hufariki lakini misimamo na matendo yao hubakia dira na nuru ya watakao kuja baada yao.

Tunaipa pole familia ya marhum na kuiombea kwa Allah awape moyo wenye kusubiri na kuwalipa kwa ujira wao In Shaa Allah wakati huu wa huzuni. Nasi hatuna la kusema ila lile analoridhia Mola wetu: *Inna lillah wa ina ilaihi raji'oon*.

Kwa hakika nyoyo zetu zimejaa huzuni na macho yakitoa machozi kwa kuondokewa na ndugu yetu,twamuomba Mola amsamehe na kumrehemu na kumweka mahala pema peponi. Ewe Allah twakuomba ukirimu mashukio yake na kukunjua kaburi lake na umpe nyumba bora zaidi kuliko aliyokuwa nayo duniani na nasi tukawe naye chini ya bendera ya Mtume (saw) siku ya Qiyama.

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari Hizb ut Tahrir Kenya**

# Miaka 97 ya Kuomboleza na Kutaabika Chini ya Idhilali ya Ukoloni wa Urasilimali



Kwa takriban miaka 1300 ya kuishi chini ya usimamizi wa Khilafah, Umma huu ulifurahia amani, utulivu na ufanisi katika muda wote huo. Lakini, kila kitu kilikoma mnamo 28 Rajab 1342 H sawia na 3 Machi 1924 pindi wanafiki na wapatilizaji fursa walipotongozwa na thaqafa ya kikafiri na kuvutiwa na mfumo wake wa kimaisha wakiongozwa na Mustafa Kamal. Walitekeleza njama za Wamagharibi, waliotaka kuvunjwa kwa Khilafah wala kutosazwa chochote katika ukumbusho wake kwani huenda kikawa kichocheo cha Mwamko wa Kiislamu. Walifaulu katika kuiondoa Khilafah lakini, Imani ya Waislamu na Dini yao haikuondolewa badala yake ilichochea wimbi la uchukivu kwani ni kinyume na Uislamu kuishi pasi na Khilafah kwa kuwa ndio ngao ya Umma huu na hivyo mambo yake husimamiwa na kupelekwa kwa mfumo huu wa Kiislamu. Kama ilivyo simuliwa kuwa Rasulullah (saw) asema:

انما الإمام جنة يقاتل من ورائه ويتقى به

**Hakika, Imam ni ngao, watu hupigana nyuma yake na kujihami nayoIndeed.** [Muslim]

Wamagharibi kupitia mfumo wao muovu wa kirasilimali mpaka leo wanaendelea kusababisha ghasia katika ardhi zote za Waislamu na kuugawanya Umma ambao mwazoni uliungana pamoja kuwa vijidola vidogo vidogo kila mojawapo kikitawaliwa na mtawala kibaraka wa wakoloni anaye zungukwa na duara la wasaidizi wake ambaye Qibla chake ima kiko London au Washington. Watawala hawa vibaraka wa wakoloni kwa usaidizi kutoka kwa mabwana zao wameleta maafa baada ya maafa. Maafa haya yanajumuisha miongoni mwa mengine kuupa Uislamu sura mpya ya kileo ili ukubaliane na maadili ya mabwana zao wa Kimagharibi, wakiwabandika majina na kuwafunga gerezani Waislamu wanaolingania mwamko wa Kiislamu kuwa magaidi au waliovuka mipaka. Wakitabikisha kila aina ya sera zinazo ashiria ushawishi wa Wamagharibi kwa vidola hivyo katika sekta zote kuanzia biashara – zinazo endeshwa kwa misingi ya riba, jamii inayo endeshwa kwa misingi ya uhuru, na siasa bandia – zisokuwa na sera ya kigeni na viwanda – vinavyo endeshwa kwa misingi ya ubinafsishaji nk.

Watawala vibaraka hawa walisonga mbele zaidi katika kuwaabudu mabwana zao kufikia kiwango cha kutoa nafasi kwa amali za majeshi ya Kimagharibi zilizo lengwa ndugu zao huku wakijitia upofu wanapo elekezwa kuangalia uharibifu wanaoutekeleza. Maisha yamekuwa magumu mno chini ya idhilali ya watawala vibaraka wa wakoloni ambao wako katika hali ya wazimu na kutapatapa kuokoa viti vyao mamlakani kupitia kumaliza tishio lolote la hali halisi yao. Huku ulinganizi wa mwamko wa Kiislamu ukifikia kilele chake, imepelekea watawala vibaraka na mabwana zao wakoloni kuwahadaa watu kwa kuuonesha Uislamu kama mfumo katili, ambao hauwezi kuwa badili ya mfumo batili wa kirasilimali. Wamefaulu katika kujidanganya wenyewe na wale walioko pambizoni mwao ama kwa wengi wa watu wakiwemo wale walioko eneo la Magharibi na ulimwengu mzima wa Kiislamu kamwe hawaja kubali ujanja wao na kwa hivyo njama zinafichuka mbele ya macho yao huku watu wakisilimu na ulinganizi wa mwamko ukizidi kufikia kileleni kila uchao kwa fadhila na rehma za Allah (swt):

Endelea Uk..5



Email: info@uqab.or.ke

كَتَبَ اللَّـهُ لَأَغْلِبَنَّ أَنَا وَرُسُلِي ۚ إِنَّ اللَّـهَ قَوِيٌّ عَزِيزٌ
“**Allah ameandika: Hapana shaka! Mimi na Mitume yangu tutashinda. Hakika Allah ni Mwenye nguvu, Mwenye kushinda.**” [Al-Mujaadalah: 21]

Hakika, kwa miaka tisiini na saba, tumekuwa tukiomboleza na kutaabika chini ya idhilali ya ukoloni wa urasilimali; kuanzia Mashariki ya Kati, Afrika, Asia, Latin Amerika nk. Watu wametabanni mwito wa maisha uchungu unaosema: ‘jana ilikuwa bora kuliko leo’ huku majambazi wa kirasilimali na makampuni yao ya kimataifa wakiwatafuna kila uchao kwa sera za kinyama zinazo lenga kuwatapeli rasilimali zao nyingi. Kila dakika inasonga kwa kufichuka kwa majaribio tasa ya kujaribu kuuokoa uhalisia wa kuporomoka kwa mfumo muovu wa kisekula wa kirasilimali unaosubiri mazishi wakati wowote hivi kuanzia sasa. Nyoyo zetu zinapiga kwa macheo mapya, ambayo dalili zote zinaashiri kukaribia kwake kwa kasi. Macheo haya mapya chini ya uongozi wa Khilafah itakayo simamishwa katika njia ya Mtume (saw) hayana shaka kama ilivyo bashiriwa na Mtume Muhammad (saw) katika hadith maarufu:

**…kutakuwepo na tawala za kiimla kwa muda apendao Allah kuwepo kwake.**[Ahmad]

Zaidi ya hayo, Allah (swt) ameahidi ushindi:

وَعَدَ اللَّـهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَـٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ

“**Allah amewaahidi wale walio amini miongoni mwenu na wakatenda mema, ya kwamba atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyo wafanya makhalifa wa kabla yao, na kwa yakini atawasimamishia dini yao Dini yao aliyo wapendelea, na atawabadilishia amani baada ya khofu yao. Wawe wananiabudu Mimi, wala wasinishirikishe na chochote. Na wakao kufuru baada ya hayo, basi hao ndio wapotovu**”. [Nur: 55]

Na Yeye (swt) pia anasema:

وَلَا تَهِنُوا وَلَا تَحْزَنُوا وَأَنتُمُ الْأَعْلَوْنَ إِن كُنتُم مُّؤْمِنِينَ
“**Wala msilegee, wala msihuzunike, kwani nyinyi ndio wa juu (washindi) ikiwa nyinyi ni waumini (wa kweli)**”.
[Al-Imran: 139]

Kwa bishara ya Rasulullah (saw) na ahadi kutoka kwa Allah (swt) Umma wa Kiislamu ni lazima kutokaa na kungoja tu mambo yajitokeze, badala yake, ni lazima tubakie imara na wakakamavu katika ulinganizi wetu wa mwamko wa kweli wa Kiislamu unaolenga kurudisha mfumo kamili wa Kiislamu kupitia kusimamisha tena Khilafah kwani ni kupitia kwayo pekee ndio hadhi ya Umma huu na heshima yake itakapo patikana. Khilafah itawakomboa sio tu Waislamu pekee bali pia Wasiokuwa Waislamu na wanadamu wote kwa jumla kutokana na njama za mfumo batili wa kikoloni wa kisekula wa kirasilimali na nidhamu zake zinazo nuka zitokamanazo nao ikiwemo nidhamu ya kiutawala ya kijambazi ya Kidemokrasia. Allah (swt) asema:

وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا رَحْمَةً لِّلْعَالَمِينَ
“**Na hatukukutuma (Ewe Muhammad), isipokuwa uwe ni rehma kwa walimwengu wote**”.
[Al-Anbya: 107]

Wakati umewadia sasa mujiunge ikiwa bado hamujafanya hivyo na kazi ya kulingania ukombozi wa kweli unaoongozwa na Hizb ut Tahrir, chama cha kisiasa cha Kiislamu ambacho hakiogopi wala kuficha maneno yake dhidi ya watawala vibaraka wa wakoloni na mabwana zao wakoloni inapo kuja katika kuamrisha mema (kheri) na kukataza maovu (munkar) huku macho yake yakiangazia na kulenga kusimamisha tena Khilafah Rashidah katika njia ya Mtume (saw).

**Enyi Vijana wenye ikhlasi wa Umma wa Kiislamu,**

Ambao kwa sasa muko katika kambi za kijeshi, ndugu zenu na dada zenu nchini Kashmir, Palestina, Syria, Somalia nk, wanawalingania kuipa Nusra (usaidizi wa kijeshi) Hizb ut Tahrir kusimamisha Khilafah ambayo itawakomboa kutokana na mateso yao na kwayo itaunganisha Umma huu, majeshi yake na ardhi zake na kuanza kulingania Da’wah ya Kiislamu ulimwengu mzima. Je, hamupendi kutambuliwa kama Saad ibn Mu’adh (ra) alivyo kuwa pindi alipo fariki arshi ya Allah ilitingishika na ambaye milango ya pepo ilifunguliwa kwa ajili yake na mazishi yake kushuhudiwa na malaika ambao hawaja wahi kushuka ardhini isipokuwa siku hiyo na kwenda haraka kwa ajili ya kushindana katika kushiriki katika mazishi yake na kupata daraja yake kwa heshima na unyenyekevu kwake? Au mumechagua kutumiwa kama vikaragosi katika vita vya wakala vya kiulimwengu ambavyo matunda yake ni fedheha duniani na Jahannam kesho Akhera? Macheo yamewasili baada ya miaka 97 Allah (swt) angali amewapa fursa muandikwe katika historia kama alivyo kuwa Khalid bin Walid (ra). Zikomboeni nafsi zenu kutokana na utiifu kwa watawala vibaraka wa wakoloni na kumbatieni mwito wa Allah (swt) na Mtume wake (saw):

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اسْتَجِيبُوا لِلَّـهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُمْ لِمَا يُحْيِيكُمْ ۖ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّـهَ يَحُولُ بَيْنَ الْمَرْءِ وَقَلْبِهِ وَأَنَّهُ إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ
“**Enyi mulio amini! Muitikieni Allah na Mtume anapo kuitieni jambo la kukupeni uzima wa milele. Na jueni kuwa Allah huingia kati ya mtu na moyo wake, na kwamba hakika kwake Yeye tu mtakusanywa**”.
[An-Anfal: 24]

Imeandikiwa Afisi ya Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya**

# Tuongezeni Juhudi Zetu Maradufu Katika Kuifanyia Kazi Mama wa Faradhi Zote




Tarehe 28 Rajab 1439 itakuwa ni kumbukumbu ya kuondolewa kwa Khilafah. Mmoja katika watoto watukufu wa Ummah huu Kathim Qara Bakir, Jenerali wa Khilafah ya Kiuthmania, alisema, “Nimeapa kuzuia hatua zozote zitakazo chukuliwa kwa lengo la kuibadilisha nchi hii kutoka kuwa Usultan mpaka kuwa jamhuri, hata kama kujitolea muhanga huko kutakuwa ghali kiasi gani”. Mustafa Kamal msaliti, msekula alisimama dhidi ya maneno haya mazito ya jenerali huyo na kufanya kazi pasi na kuchoka kusababishia ulimwengu wa Kiislamu uhalisia mchungu yaani kuvunjwa kwa Khilafah. Tukio hili lilitokea jijini Istanbul mnamo 28 Rajab 1342 H ikiafikiana na tarehe 3 Machi, 1924 ni mojawapo ya matukio ya kuchukiza mno katika historia ya Kiislamu.

Ndio, hakika kuondolewa kwa Khilafah kulisababisha kuzuka kwa majanga ndani ya ulimwengu wa Kiislamu na ulimwengu mzima kwa jumla. Ummah huu mtukufu kwa sasa unaishi chini ya idhilali ya ufisadi wa urasilimali na unakabiliwa na ugandamizaji, ufukara na baya zaidi ni kutohukumu au kutotekeleza Sharia ya Allah, Muumba wa Ulimwengu! Kibla chetu kimegeuka na kuelekea Washington ambako maagizo na amri zinatolewa kwa ajili yetu. Ardhi zetu zinatawaliwa na Ruwaibidha ambao pamoja na mabwana zao hawaleti chochote ila fedheha. Ummah huu umo ndani ya faudha kikamilifu. Baya zaidi ni yale yanayo shuhudiwa nchini Syria kwa sasa a**rdhi ambayo Mtume (ﷺ) aliita al-Sham twahara zaidi katika ardhi za Allah, sehemu ambayo dini, Imani na usalama zinapatikana katika nyakati za mzozo**. Ardhi ambayo Waislamu chini ya uongozi wa Umar (ra) ilifaulu katika kuifungua ile inayojulikana Syria ya leo na maeneo pambizoni mwake. Syria kwa sasa ni eneo linalo waka moto. Vita sasa vimefikia takriban muongo mmoja, kutokana na hisia ya unyanyasaji unaofanywa juu ya Waislamu kwa zaidi ya miongo minne chini ya katili wa kiimla wa Kibaathi Bashar al-Assad aliye mrithi babake al-Hafidh katika utekelezaji uovu. Amerika pamoja na Urusi zinashambulia kutoka angani, ardhini na baharini. Maelfu wakimemo kina mama na watoto wameuwawa. Hali nchini Syria imepelekea kutokea kwa janga la wakimbizi la viwango vikubwa mno, ambavyo havijawahi kushuhudiwa tangu Vita vya Pili vya Dunia.

Hakika ni kwa kukosekana Khilafah ndipo taswira za umasikini, baa la njaa, ukame na la kusikitisha zaidi vita vya wenyewe kwa wenyewe vinaonekana kama nembo za Afrika. Tangu kinyang’anyiro cha wakoloni wa ulaya kwa bara la Afrika cha madini na rasilimali nyingi za bara hili katika karne ya 20, bara hili tajiri lilifanywa kuwa tu mkondo wa usambazaji kwa falume zao. Ni kinaya, kwa Donald Trump kuiita

*Endelea Uk..7*

Afrika kuwa nchi za mashimo ya kinyesi. Chini ya urasilimali, kilio cha Afrika leo kiko mbali na ilipokuwa siku za nyuma. Kuiangalia kwa upesi historia ya Afrika chini ya Khilafah, ingawa si Afrika yote ilitawaliwa na Khilafah bali ni baadhi ya sehemu tu za bara hili zilizofunguliwa na Khilafah. Kufikia katikati mwa karne ya 6 mpaka karne ya 7 kwa mfano, Afrika Kaskazini ilikuwa tayari ishafunguliwa na Khilafah hivyo basi miji mikuu mingi kama Tripoli – Libya, Tunis – Tunisia ilikuwa ikidhibitiwa na Waislamu. Miji yote hii kwa ujumla ilikuwa ikijulikana kama mikoa ya Kirumi barani Afrika. Katika eneo la Mashariki mwa Afrika, mwanga wa Khilafah ulionekana wakati wa Khilafah ya Abdul Malik bin Marwan, sehemu za Somalia ya leo ikiwemo Mogadishu, zilikuwa chini ya kivuli cha Dola ya Kiislamu. Hili lilichangia kuenea kwa Uislamu katika baadhi ya miji ya mwambao wa pwani kama Mombasa, Dar es-salaam, Zanzibar, Kilwa na Msumbiji.

Kuondolewa kwa Khilafah kulimaanisha kuyafungua mafundo ya Uislamu.

Abu Umamata Al-Baahili amesimulia kuwa Mtume (saw) amesema:

لَيُنْقَضَنَّ عُرَى الْإِسْلَامِ عُرْوَةً عُرْوَةً فَكُلَّمَا انْتَقَضَتْ
عُرْوَةٌ تَشَبَّثَ النَّاسُ بِالَّتِي تَلِيهَا وَأَوَّلُهُنَّ نَقْضًا الْحُكْمُ
وَآخِرُهُنَّ الصَّلَاةُ

**Mafundo ya Uislamu yatafunguka moja baada ya moja, kila fundo moja litakapo funguka watu wataligwia fundo jengine, na fundo la kwanza kufunguka ni Hukmu na la mwisho kufunguka ni Swala** (Imeripotiwa na Hakim na Ahmed)

Ndio, kwa hakika kuwepo kwa Khilafah kuliyafanya mafundo ya Uislamu kufungika imara. Hakuna damu iliyo mwagwa pasi na hatia.

Kuendelea kuyahesabu majanga baada ya kuvunjwa Khilafah hakuta yasitisha vile vile kukumbuka kuvunjwa kwake hakupasi kuchukuliwa kama matanga bali kuwe ni kichachawizo cha Ummah kuongeza juhudi zake maradufu katika kufanya kazi ya kuisimamisha tena. Ulinganizi wa Khilafah kwa sasa unahisika ndani ya mishipa ya Waislamu kote duniani. Wamagharibi wanazipa nguvu upya juhudi zao za kuzuia kurudi kwa Khilafah. Hawana budi kujua kwamba Uislamu ni Khilafah na Khilafah ni Uislamu, ambayo Allah (swt) amewaahidi waumini Wake.

وَعَدَ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ مِنكُمْ وَعَمِلُوا۟ ٱلصَّٰلِحَٰتِ
لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِى ٱلْأَرْضِ كَمَا ٱسْتَخْلَفَ ٱلَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ
وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ ٱلَّذِى ٱرْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّنۢ
بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِى لَا يُشْرِكُونَ بِى شَيْـًٔا ۚ وَمَن
كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْفَٰسِقُونَ

**Allah amewaahidi wale walio amini miongoni mwenu na wakatenda mema, ya kwamba atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyo wafanya makhalifa wa kabla yao, na kwa yakini atawasimamishia dini yao Dini yao aliyo wapendelea, na atawabadilishia amani baada ya khofu yao. Wawe wananiabudu Mimi, wala wasinishirikishe na chochote. Na wakao kufuru baada ya hayo, basi hao ndio wapotovu.** [Nur: 55]

Ndiyo, Khilafah ni ahadi ya Allah (swt) ambayo inakuja hivi karibuni na hakuna wa kuizuia. Tunamuomba Allah (swt) katika mwezi huu mtukufu wa Rajab ambao tunakumbuka tukio hili baya na chungu la kuvunjwa kwa Khilafah kuturuzuku nguvu zaidi za kufanya kazi kwa ajili ya kuisimamisha tena kwa idhini ya Allah.

Imeandikiwa Afisi ya Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut Tahrir Kenya**

# Hatimaye, Viziba Uso Vimeanguka kutoka Nyusoni mwa Vibaraka wa Marekani, Erdogan, Rouhani na Putin. Wameshughulishwa na uwakala wa kuhakikisha wanamhifadhi kibaraka wa Marekani ndani ya Syria, ili Marekani imakinike kutatua Janga la Korea na China

Siku ya Jumatano 04/04/2018, maraisi wa Urusi, Iran na Uturuki walikutana mjini Ankara, na kutoa kauli yao ya mwisho. Ilikuwa wazi kutokana na kauli hiyo, ima kupitia kauli ya maandishi au kwa yaliyofichika…kwamba wao watatu wameamua kuhakikisha wanaudhibitisha utawala wa kibaraka wa Marekani ndani ya Syria, na kusitisha muamko wa watu wa Syria wa kutaka kusimamisha utawala wa Kiislamu.

Ama kwa Erdogan, alitumia khiyana na kuendelea kufanya hivyo, ndani ya Oparesheni ya Euphrates Shield, na kuunganisha wapiganaji kuelekea ngao yake, ambapo Aleppo ilianguka na kukabidhiwa utawala. Kisha ikaja Oparesheni Olive Branch, ambapo aliwaunganisha wapiganaji kwenda Afrin na kusini mwa Idlib kukaanguka, ikafuatiwa na mashariki mwa Ghouta…Bado ana "Ngao" na "Matawi" aliyoyaficha mpaka amalize kuwaunganisha wapiganaji ndani ya Idlib, na kisha awaunganishe katika eneo jengine, mwishowe Idlib itaanguka!

Ama kwa Rouhani-Khamenei, wanamgambo wake nchini Syria wamezagaa katika milima na majangwa, kuanzia kitengo cha ulinzi cha mapinduzi na chama chake cha Lebanon, mpaka wanagambo wake wa angani. Wote wanatoa kila juhudi kuuwa watu ili kumdhibiti dhalimu wa Ash-Sham.

Ama kwa Putin, uhalifu wake ndani ya Syria uko wazi kwa kila mmoja kuona, na hauhitaji khiyana kuuonyesha, kama wanavyofanya Erdogan au Rouhani-Khamenei. Wanatumia khiyana, kwa sababu wanapiga kelele za juu kwamba ni Waislamu! Putin hahitaji kufanya hivyo, anajulikana kama adui wa Uislamu na Waislamu.

Hawa watatu wameshughulishwa na kudhibiti utawala wa kisekula wa kibaraka wa Marekani ndani ya Syria na wanatekeleza uhalifu, uuaji na ukatili ndani ya Syria, walioko katika mamlaka yao na hata zaidi ya nguvu zao! Wanajua kwamba serikali hii inaendeshwa kwa msukumo wa Marekani, na kwamba kuimakinisha kiwakala ni kuiruhusu Marekani kuweza kupambana na majanga ya Mashariki ya Asia ndani ya Korea Kaskazini na China… Lau wangelikuwa na busara wangelifuata mtizamo mwengine kuliko huu, lakini Shetani anawadhibiti wafuasi wake.

Hata hivyo, wahalifu hawa, ima wamekuwa watatu au Marekani ipo nyuma yao, wasingeliweza kuwa na msimamo kwa uhalifu wao lau isingelikuwa kwa idadi ya makundi yanayowafuata, kwa mujibu wa sera ya kurambisha ya kupeana karoti na nifuate, iliyofungamanishwa na pesa chafu, vitisho na kuogofya, ingelikuwa si hivyo wahalifu hao wangelifeli.

Japo Hizb ut Tahrir imemaliza kila juhudi katika kujaribu kuleta muamko ndani ya makundi haya, kutokana na yanayoendelea, bado wanakimbilia njia hiyo kwa kisingizio cha kupata pesa na silaha, na kwamba Hizb ut Tahrir haiwezi kufanya hivyo bali wanawaunga mkono kwa ushauri… Wakaongezea kuwa ushauri hautoshi katika vita vya silaha! Hawakujua kwamba upanga wao una pande mbili, ni ngao katika mkono wa aliye na muamko na wenye utambuzi kutoka katika uovu wa adui wake, na zana yenye nguvu kumshinda adui wake…Lakini ngao hii ina makali wakati imo mkononi mwa aliye danganywa, akikimbilia msaada wa wahalifu, pande zake zilizovunjika zinawaua wafuasi wake mbele ya adui!

Twayaambia makundi haya yaliyopinga ushauri wetu na muamko; walisema kuwa haya hayato wasaidia katika vita, na wakachagua msaada wa pesa na silaha kutoka kwa wasaliti wa Waislamu, Waarabu, Waturuki na Wafursi, wengine wakaongezea kuwa watachukua hata kutoka kwa wahalifu wa Kimarekani na Kirusi. Wakifikiria kuwa kuchukua kwao pesa chafu kutawafanya kutositisha mapigano kwa ajili ya Ash-Sham… Twawaambia wote: Sasa mwaona matokeo ya vitendo vyenu na maneno yenu, mumetenganishwa na kufurushwa kutoka majumbani mwenu na watoto!

Hata hivyo, Ummah huu hautoshindwa, kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu mambo yatabadilika. Ummah huu umefikwa na majanga na zaidi ya hayo ni kutoka kwa vita vya Msalaba na Tatar, na ulinyanyuka na kuwang'oa na kuwa kileleni mwa dunia tena. Ni kweli utawala wa Uislamu ulikuwa umesimamishwa nyakati hizo, na kwamba Khilafah ilikuwepo licha ya udhaifu wake, bado Ummah ulikuwa na kiongozi aliyewaunganisha katika kupigana na adui, na kusimamisha ukweli na kuangamiza uongo, na kisha ukamshinda adui na kuinuka tena… Leo hakuna utawala wa Uislamu, hakuna Khilafah, hivyo basi, nani atakayewaunganisha Waislamu kupigana?

Hakika mtu anaweza kusema hivi, ni upi uchanganuzi wa hali halisi, lakini kazi ya kuregesha Khilafah inaendelea kwa nguvu, kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu. Imekuwa hitajio kubwa kwa Waislamu ndani ya nchi zao, na wanatamani kwa

*Endelea Uk..9*

maneno na vitendo, na wanafanya kazi kubadilisha siku nyeusi za 26, 27 na 28 za Rajab 1342H, ambazo zilikuwa jukwaa la ukhaini na uhalifu katika kuvunja Khilafah. Wanawania kuziondosha siku hizo nyeusi, na kuweka badala yake Khilafah tena, katika siku iliyochaguliwa na Mwenyezi Mungu, na ni jambo jepesi kwa Mwenyezi Mungu kulitekeleleza hili, na kisha wale waliokosa, waliosaliti na kufanya uhalifu watajua hatima yao.

**Enyi Waislamu:** Hao watatu waliotekeleleza uhalifu dhidi ya Syria, Makafir na wanafiq miongoni mwao hawatofurahi katika uhalifu na mauaji yao dhidi ya watu wa Ash-Sham na watu wake, lakini adhabu yao itakuja kutoka wasiko kutarajia. Ash-Sham imejaa mfano wao lakini bado imesimama, na wameangamia. Na hivi ndivyo itakavyokuwa kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu (swt)

إِنَّ اللَّهَ بَالِغُ أَمْرِهِ قَدْ جَعَلَ اللَّهُ لِكُلِّ شَيْءٍ قَدْرًا

"**Hakika, Mwenyezi Mungu anatimiza amri yake. Mwenyezi Mungu kajaalia kila kitu na kipimo chake**" [At-Talaq: 3].

Mwisho, huu ni ujumbe kwa majeshi ya Waislamu yaliyomo ndani ya kambi… Hali yenu inashangaza, mkitumwa na watawala mkawaue Waislamu munatwii, na Waislamu wanapowalilia kutaka msaada wenu, mnasita na kuwaangusha na kubakia kimya mfano wa kimya cha kaburi. Na mnatoa hoja kuwa mnatwii wakuu wenu, ilhali hii ndiyo barabara inayowapelekea katika hizaya duniani na adhabu chungu Yaumul Qiyama, na hao (watawala) hawatowasaidia siku hiyo, lau mtazungumza mkijitetea:

يَوْمَ تُقَلَّبُ وُجُوهُهُمْ فِي النَّارِ يَقُولُونَ يَا لَيْتَنَا أَطَعْنَا اللَّهَ وَأَطَعْنَا الرَّسُولَا * وَقَالُوا رَبَّنَا إِنَّا أَطَعْنَا سَادَتَنَا وَكُبَرَاءَنَا فَأَضَلُّونَا السَّبِيلَا

"Siku ambayo nyuso zao zitapinduliwa pinduliwa katika Moto. Watasema: Laiti tungeli mtii Mwenyezi Mungu na tungeli mtii Mtume! Na watasema: Mola wetu Mlezi: Hakika sisi tuliwatii bwana zetu na wakubwa wetu; nao ndio walio tupoteza njia." [Al-Ahzab: 66-67]

Hata hivyo, bado munao muda wakuweza kuyabadili muliyo yafanya, kwa kuinusuru Dini ya Mwenyezi Mungu, kuurudisha utawala wa Uislamu katika ardhi, na kukata mahusiano na wadhalilishaji na wanafiki, na Makafiri wakoloni. Hili liwe kafara kwa madhambi yenu, na Mwenyezi Mungu ni mkweli alisema:

وَإِنِّي لَغَفَّارٌ لِمَنْ تَابَ وَآمَنَ وَعَمِلَ صَالِحًا ثُمَّ اهْتَدَى

"**Na hakika Mimi ni Mwingi wa Kusamehe kwa anaye tubia, na akaamini, na akatenda mema, tena akaongoka.**" [Ta-Ha: 82].

Kwa kuongezea, twataka kusema kwa Waislamu jumla, musikate tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu, Ash-Sham itabakia kuwa Ash-Sham, nyumba tukufu ya Uislamu. Ahmad katika simulizi yake alieleza kutoka kwa Jubair Bin Nafir, kwamba Salma bin Nufail, aliwaambia kuwa alikwenda kwa Mtume (saw), na Mtume (saw) akamwambia:

أَلَا إِنَّ عُقْرَ دَارِ الْمُؤْمِنِينَ الشَّامُ

"**Hakika nyumba ya waumini ni Ash-Sham**"

Katika simulizi nyingine ya Na'im Bin Hammad kuhusiana na mzozo, kutoka kwa Katheer Bin Murrah, alisema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) alisema:

عُقْرُ دَارِ الْإِسْلَامِ بِالشَّامِ

"**Ash-Sham ni nyumba ya Uislamu**".

Tukimalizia, Hizb ut Tahrir, muongozaji asiyedanganya watu wake, inaendelea na kazi yake pamoja na kupitia Ummah, na iko imara katika ukweli, kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu. Hayakubadilika na haitobadilisha mawazo na njia yake, maanake ni ya ukweli.

فَمَاذَا بَعْدَ الْحَقِّ إِلَّا الضَّلَالُ

"**Na kipo kitu gani baada ya haki, isipokuwa upotovu tu?**" [Yunus: 32]

Chama kina nguvu kwa msaada wa Mwenyezi Mungu na Dini, kinamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu na Mwenye Hekima, kwamba ahadi ya Mwenyezi Mungu itimizwe kwa mikono yake.

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ

"**Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walio amini miongoni mwenu na wakatenda mema, ya kwamba atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyowafanya makhalifa kabla yao,**" [An-Nur: 55].

Na bishara ya Mtume (saw) itatimizwa na chama na watu wake, na Waislamu wote. Abu Daoud At-Tialsi asimulia kutoka kwa Hudhayfah kwamba alisema kwamba: Mtume (saw) alisema:

ثُمَّ تَكُونُ جَبْرِيَّةً، فَتَكُونُ مَا شَاءَ اللَّهُ أَنْ تَكُونَ، ثُمَّ ... يَرْفَعُهَا إِذَا شَاءَ أَنْ يَرْفَعَهَا، ثُمَّ تَكُونُ خِلَافَةً عَلَى مِنْهَاجِ النُّبُوَّةِ، ثُمَّ سَكَتَ

"kisha kutakuwepo na ukandamizaji kwa muda atakao Mwenyezi Mungu, kisha atauondosha Atakapotaka, na kisha kutakuwepo na Khilafah kwa njia ya Utume" na kisha akabakia kimya" Na Ahmad akatoa kutoka katika mfano huo: Mtume (saw) alisema:

ثُمَّ تَكُونُ مُلْكًا جَبْرِيَّةً، فَتَكُونُ مَا شَاءَ اللَّهُ أَنْ ... تَكُونَ، ثُمَّ يَرْفَعُهَا إِذَا شَاءَ أَنْ يَرْفَعَهَا، ثُمَّ تَكُونُ خِلَافَةً عَلَى مِنْهَاجِ نُبُوَّةٍ» ثُمَّ سَكَتَ

"kisha kutakuwepo ufalme wa ukandamizaji kwa muda atakao Mwenyezi Mungu, kisha atauondosha Atakapotaka, na kisha kutakuwepo Khilafah kwa njia ya Utume" na kisha akabakia kimya"

Hizb ina uhakika wa ushindi kutoka kwa Mwenyezi Mungu, si tu kwa mitume na manabii, bali pia kwa waumini wa kweli, si tu Akhera, bali pia hapa duniani,

إِنَّا لَنَنْصُرُ رُسُلَنَا وَالَّذِينَ آمَنُوا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيَوْمَ يَقُومُ الْأَشْهَادُ

"**Hakika bila ya shaka Sisi tunawanusuru Mitume wetu na walio amini katika uhai wa duniani na siku watakapo simama Mashahidi,**" [Ghafir: 51]. Siku hiyo, waumini watafurahi kwa ushindi wa Mwenyezi Mungu, na wahalifu watapata hizaya hapa duniani, na adhabu chungu Akhera. Mwenyezi Mungu ni muweza katika kulipiza [Al-Muntaqim], Ni Mwenye Nguvu na Hekima

H. 18 Rajab 1439
M. : Alhamisi, 05 Aprili 2018



# Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi

# Halaqa 12: Mapambano ya Kisiasa Katika Da’wah ya Mtume (saw

Katika halaqah hii tunaendelea na hatua ya tatu katika njia ya Mtume (saw) kuleta mageuzi. Leo tutazungumzia kuhusu mapambani ya kisiasa katika da’wah ya Mtume (saw).

Mapambano ya kisiasa ni kuwabishia milango mabwenyenye na viongozi. Na walio katika wanasiasa na wanaotawala watu, nayo ni kupambana nao kwa fikra pekee bila kutumia mabavu, wala mgongano wa kuendelea wa Kisilaha.

Mapambano ya kisiasa yanakuwa kwa kufichua mipango ya watawala, na kufichua njama zao na khiyana zao. Kwani walijaribu maswahaba wa Mtume (saw) wakiongozwa na Umar ibnul Khatwwab (ra) kabla kusimama kwa dola walitaka kupambana na mabwenyenye na viongozi kwa mgongano wa kudumu wa kisilaha, Na walikuwa wana kiu ya kuwapiga vita, walikuja kwa Rasulullah (saw) na wakamwambia: “**Ewe mjumbe wa Allah! Je, hatuko katika haki?**” Akasema Rasulullah (saw): “**Kwa nini? Ndio tuko katika haki**” Na wakamwambia: “**Je, wao hawako katika batil?**” Rasulullah (saw) akasema: “**Kwa nini? Wao wako katika batil**” Wakasema: “**Ewe mjumbe wa Allah kwa nini tuidunishe dini yetu...? Ewe Mtume wa Allah! Tupe amri kesho tuwashambulie hawa jamaa kwa panga zetu...!**” Mtume (saw) akawaambia: “**Hapana bado hatujaamrishwa hivyo**”. Kwa mfano wa jambo kama hili lahitaji ruhusa kutoka kwa mtungaji sheria Allah, Taa’la.

Na hakika iliweza kupatikana baada ya kusimama dola ruhusa ya kupigana; Akasema Taa’la:

أُذِنَ لِلَّذِينَ يُقَاتَلُونَ بِأَنَّهُمْ ظُلِمُوا ۚ وَإِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ نَصْرِهِمْ لَقَدِيرٌ

Wameruhusiwa kupigana wale wanao pigwa vita kwa sababu wamedhulumiwa - na kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kuwasaidia [Al-Hajj: 39]

**Mapambano ya Kisiasa Yalivyokuja Katika Qur’an na Mtume (saw) Kuyafanya Kabla ya Kusimama Dola:**

Ama kabla ya kusimama dola, alikuwa Rasulullah (saw) akiwasafihi waerevu wao majahili akiwasifu kuwa ni waongo, wapakaji mafuta. Na mara nyingi akiwatisha bila ya kupigana, na hakutaka kwa yoyote miongoni mwa maswahaba wake kuwapiga vita mushrikina pamoja na kuwa wanaudhia sana.

Mtume (saw) alipambana mapambano ya kisiasa kivitendo yeye mwenyewe, ikawa anawasomea:

وَدُّوا لَوْ تُدْهِنُ فَيُدْهِنُونَ

Wanatamani lau unge lainisha ili nao wakulainishie. [Al-Qalam: 9]

Na akimsomea ami yake Abu Lahab:

تَبَّتْ يَدَا أَبِي لَهَبٍ وَتَبَّ

Imeangamia mikono ya Abu Lahab, na yeye pia ameangamia.

مَا أَغْنَىٰ عَنْهُ مَالُهُ وَمَا كَسَبَ

Hayatamfaa mali yake, wala alivyo vichuma.

سَيَصْلَىٰ نَارًا ذَاتَ لَهَبٍ

Atauingia Moto wenye mwako.

[Al-Masad: 1-3]

*Endelea Uk..11*

Na akimsomea Walid bin Mughira aliyebeba bendera ya vita ya Maquresh:

ذَرني وَمَن خَلَقتُ وَحيدًا
Niache peke yangu na niliye muumba;

وَجَعَلتُ لَهُ مالًا مَمدودًا
Na nikamjaalia awe na mali mengi,

وَبَنينَ شُهودًا
Na wana wanao onekana,

وَمَهَّدتُ لَهُ تَمهيدًا
Na nikamtengezea mambo vizuri

ثُمَّ يَطمَعُ أَن أَزيدَ
Kisha anatumai nimzidishie!

كَلّا ۖ إِنَّهُ كانَ لِآياتِنا عَنيدًا
Hasha! Kwani hakika yeye alikuwa akizifanyia inadi Aya zetu!

سَأُرهِقُهُ صَعودًا
Nitamtesa kwa mateso yasio wezekana.

إِنَّهُ فَكَّرَ وَقَدَّرَ
Kwani hakika yeye alifikiri na akapima.

فَقُتِلَ كَيفَ قَدَّرَ
Basi ameangamia! Vipi alivyo pima!

ثُمَّ قُتِلَ كَيفَ قَدَّرَ
Tena ameangamia! Vipi alivyo pima!
[Al-Muddaththir: 11-20]

Na akimsomea (saw) kinara wa ukafiri, Abu Jahli:

كَلّا لَئِن لَم يَنتَهِ لَنَسفَعًا بِالنّاصِيَةِ
Kwani! Kama haachi, tutamkokota kwa shungi la nywele!

ناصِيَةٍ كاذِبَةٍ خاطِئَةٍ
Shungi la uwongo, lenye makosa!

فَليَدعُ نادِيَهُ
Basi na awaite wenzake!

سَنَدعُ الزَّبانِيَةَ
Nasi tutawaita Mazabania!
[Al-Alaq: 15-18]

Na akimsomea Umayya Bin Khalaf :

وَضَرَبَ لَنا مَثَلًا وَنَسِيَ خَلقَهُ ۖ قالَ مَن يُحيِي العِظامَ وَهِيَ رَميمٌ
Na akatupigia mfano, na akasahau kuumbwa kwake, akasema: Ni nani huyo atakaye ihuisha mifupa nayo imekwisha mung'unyika?

قُل يُحييهَا الَّذي أَنشَأَها أَوَّلَ مَرَّةٍ ۖ وَهُوَ بِكُلِّ خَلقٍ عَليمٌ
Sema: Ataihuisha huyo huyo aliye iumba hapo mara ya mwanzo. Na Yeye ni Mjuzi wa kila kuumba.
[Yasiin: 78-79]

Alikuja Umayya kwa Rasulullah (saw) amebeba mkononi mwake mifupa iliyo oza akawa anaitifua, na kuipulizia katika uso wa Mtume (saw) na kusema: "Ewe Muhammad, Je Mola wako ataifufua hii mifupa baada ya kuoza Na kuwa mchanga...?" Mtume (saw) akajibu: "**Ndio, Allah atakufufua na akutie Jahannam**", ikawa hili ni jibu lenye kuathiri kutoka kwa Mtume (saw) akifuata amri ya Allah iliyokuja katika Kauli yake:

فَأَعرِض عَنهُم وَعِظهُم وَقُل لَهُم في أَنفُسِهِم قَولًا بَليغًا
Basi waachilie mbali, uwape mawaidha na uwaambie maneno ya kuathiri na kuingia katika nafsi zao.
[An-Nisaa: 63]

Na alikua akimsomea Walid bin Mughera':

وَلا تُطِع كُلَّ حَلّافٍ مَهينٍ
Wala usimt'ii kila mwingi wa kuapa wa kudharauliwa,

هَمّازٍ مَشّاءٍ بِنَميمٍ
Mtapitapi, apitaye akifitini,

مَنّاعٍ لِلخَيرِ مُعتَدٍ أَثيمٍ
Mwenye kuzuia kheri, dhalimu, mwingi wa madhambi,

عُتُلٍّ بَعدَ ذٰلِكَ زَنيمٍ
Mkavu, na juu ya hayo, mshari, amejipachika tu.
[Al-Qalam: 10-13]

Na ZANIIM ni mtoto wa zina, wanasema mufassirun: ziliteremka aya hizi kwa Walid bin Mughera Kwani alikuwa anadai uqureshi na si miongoni mwao, zilipoteremka aya hizi Walid alimuendea mamake akamwambia: "Hakika Muhammad amenisifu kwa sifa tisa, zote ninazo nazitambua isipokua ya tisa, akimaanisha ZANIIM/mwanaharamu. Usipo niambia ukweli nitaipiga shingo yako kwa Upanga...!" Mamake akasema: "Hakika babako alikuwa hawezi kuwaundama wanawake, wewe ni mtoto wa yule mchunga mbuzi", hakutambua kuwa yeye ni mtoto wa zinaa mpaka zilipoteremka Aya hizi...!

Asema ibnul Abbas: "na anaye kusudiwa kuwa babake ni Akhnas ibnu Shariq".

Alikuwa Rasul (saw) anasimama kwa matendo ya kisiasa, Alikuwa akiwapa sifa watawala na wenye madaraka kwa sifa walizonazo chafu, anamsifu muongo kwa sifa ya uongo, na khaini kwa sifa za khiyana, na mnafiki kwa sifa ya unafiki, na akifichua mipango yao, na njia zao za upotoshaji.

**Itaendelea katika UQAB Toleo 17…In Shaa Allah.**

# SWALI/JAWABU:
# Uhakika wa Harakati ya Eneo la Kusini na Utiifu Wake

**Swali:**
Je, Harakati ya Kusini (Al-Hirak Al-Janoubi) bado ni Amerika? Au wakala wa baraza hilo uligeuka kuwa wa Uingereza kutokana na kudhibitiwa na Imarati na kugeuka kuwa mfuasi wa Imarati, na Imarati inawakilisha Uingereza nchini humo? Kwa maana nyengine, je, Amerika ilishindwa kuidumisha Harakati hii ya Kusini na Uingereza kupitia Imarati kuweza kuivuta upande wake? Au bado ingali ni mfuasi wa Amerika katika hatua zake, na Imarati kutokana na nguvu ya jeshi lake mjini Aden, kuweza kuishawishi pekee pasi na Harakati hii ya Kusini kuwa na utiifu kwa Uingereza?

**Jibu:**
1- Uingereza ilipata wasiwasi kugundua kuwa Amerika iliweza kuwashawishi Ali Salem Al-Beidh na Ali Nasir Mohammed kwa njia za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja kupitia Misri na Saudi Arabia katika enzi za Fahd katika miaka ya tisini mwanzoni ingawa Uingereza ndiyo iliyo unda, kupitia vibaraka wake, ile iliyoitwa "Harakati ya Kitaifa ya Ukombozi Eneo la Yemen Kusini" na kuikaribisha katika majadiliano jijini Geneva kuanzia mnamo 20/11/1967. Kisha Uingereza kulipa uhuru eneo la Kusini mwa Yemen mnamo 30/11/1967 baada ya kuondoka kwa vikosi vya Uingereza, na Al-Beidh kuwa gavana wa eneo la Kusini kwa usaidizi kutoka kwa Uingereza. Hivyo basi, uhusiano wake na Amerika ulikadiriwa na Uingereza kuwa kama fedheha! Hivyo, Uingereza ikaamua kumuondoa mamlakani, hususan kwa kuwa inao uwezo wa kufanya hivyo, kwa kule kuwa mtu wake Ali Saleh ana nguvu inayo tambulika eneo la Kusini.

Hivyo basi, vita vikazuka baina ya majeshi ya sehemu mbili hizi mnamo 1994, miaka minne tu baada ya kuunganishwa kwa sehemu mbili hizi za Yemen! Ambapo vita vilimalizika kwa kushindwa kwa majeshi yaliyo tambuliwa kama "ya Kusini", Ali Salem al-Beidh na Ali Nasser Mohammed wakatoroka, na kujitenga kando kiasi.

Wakati huo serikali ya Saleh mjini Sanaa ilikuwa imeanza kuwatesa na kuwaandama wanajeshi wa eneo la Kusini kwa miaka kadhaa. Hatimaye, shirikisho la wanajeshi wastaafu likaanzishwa eneo la Kusini, kwa hivyo kikawa ni chama chenye matakwa yanayo husiana na ugandamizaji, mateso na kunyimwa haki. Kwa kuendelea kudumu kwa dhulma hizi, hisia ya kujitenga ikapenya katika wakongwe hawa wa kijeshi waliomo ndani ya shirikisho hili, na hivyo basi kugeuka kuwa jukwaa moto la hisia ya kutaka kugawanywa kwa nchi, na kitovu cha kikundi cha wanaotaka kujitenga ambao harakati zao zilipelekea kuibuka kwa ile inayo julikana kama Harakati ya Kusini (Al-Hirak Al-Janoubi), ambayo ilijitangaza rasmi eneo la Kusini mwa Yemen mnamo 2007 kuongezea pia harakati nyenginezo zisokuwa na umuhimu sana na zenye athari hafifu ambazo hatutaziangazia juu yazo.

2- Amerika iliitumia hali hii ya eneo la Kusini kutia mguu wake eneo la Kusini mwa Yemen, kama ilivyo tia mguu wake mwengine katika eneo la Kaskazini mwa Yemen kupitia harakati ya Mahouthi na usaidizi wa Iran kwake. Hivyo basi, kwa mujibu wa mzozo wa kimataifa, Harakati hii ya eneo la Kusini imegura kutoka kwa matakwa ya kuondolewa kwa dhulma na sasa kugeuka kuwa kifaa kipya cha Amerika cha kuingilia mambo nchini Yemen ambayo serikali yake ni tiifu kwa Uingereza.

Dola kuu kama desturi yazo zimekuwa zikipatiliza hali za kindani na mivutano katika nchi ndogo kujipatia ushawishi ndani yake. Amerika, kupitia Huduma ya Ujasusi ya Mfalme Fahd nchini Saudi Arabia, ilijaribu kuwasiliana na wanamgambo eneo la Kusini mwa Yemen katika miaka ya tisini baada ya vita vya wenyewe kwa wenyewe mnamo 1994. Ingawa Salem Al-Beidh alikuwa mmoja wa wafuasi wake wakati huo, kujitenga kwake kando wakati huo na kulingania kwake shughuli ya kisilaha dhidi ya utawala wa Saleh, akiwa mafichoni mwake, hakukuifanya Amerika kuliona hilo pekee kama mafanikio na ikaanza kumtafuta mtu mwengine atakaye tabanni mapambano imara ya kisiasa ili kuwakusanya watu wa eneo la Kusini kuwa pote litakalo tia shinikizo kali na kuathiri utawala wa Saleh vilivyo. Amerika ilipata njia yake kupitia mwanaharakati wa upinzani, Hassan Baoum, ambaye alikuwa anakwenda kwa kasi mno katika kuitisha kujitenga kwa eneo la Kusini mwa Yemen, na kuraukia mji mmoja hadi mwengine, na kuyazungukia makabila kwa bidii akiyarai kumuunga mkono yeye na matakwa yake ya kujitenga. Yote hayo ni athari ya mateso na kutelekezwa kwa watu wa eneo la Kusini. Baoum alikuwa akifanya tukio moja hadi jengine ili kujenga rai jumla ya kutaka kutengwa kwa eneo la Kusini kutoka kwa Yemen, kwa kufuata mwelekeo wa amani na kupinga ghasia. Ilionekana kuwa harakati za Hassan Baoum zilikuwa zinapaza sauti na wakati mwengine kupanda kasi katika maeneo ya Kusini ambako fikra ya kutelekezwa ilikuwa imekita mizizi kama sera imara.

Alikamatwa na kushtakiwa na serikali ya Sana'a, ambapo alikamatwa mara kadhaa kwa kipindi cha zaidi ya mwaka mmoja baina ya mwaka wa 2007 na 2008. Alikamatwa tena mnamo 2010 na kuachiliwa baada ya miezi miwili mnamo 2011 na kukamatwa tena mwaka huo huo. Hivyo basi, mwanaharakati wa kujitenga, Baoum, akawa nembo kuu ya Al Hirak, harakati ya kujitenga eneo la kusini, kwa juhudi zake zisochoka, kuchochea kwake wakongwe wa kijeshi, makabila na wanaharakati dhidi ya serikali kuu jijini Sana'a, kwa kule kupanda kwake na kumakinisha matakwa ya kujitenga, mafungamano yake na Amerika na kukubali kwake usaidizi

*Endelea Uk..13*

wa Iran. Baoum amesifiwa kwa harakati za kasi, hivyo akaunda Baraza Kuu la Harakati ya Eneo la Kusini na kuwa Raisi wake. Baraza hilo Kuu la Harakati ya Amani ya Ukombozi wa eneo la Kusini ni sehemu kuu ya Al Hirak, ambayo pia inajumuisha makundi mengine yakiwemo Baraza Kuu la Kitaifa la Uhuru wa eneo la Kusini, Baraza Kuu la Ukombozi na Kuregesha Dola ya Yemen Kusini, Jumuiko la Kidemokrasia la Eneo la Kusini na Muungano wa Vijana na Wanafunzi wa Eneo la Kusini… mkoa wa Dhale ni moja ya mikoa michangamfu na maeneo moto zaidi ya Al Hirak… (Chanzo: tovuti ya Al Jazeera Net 3/3/2011). Tovuti nyenginezo zilimsifu waziwazi kuwa kibaraka wa Iran kama ilivyo tajwa katika tovuti ya hunaaden.com mnamo 13/9/2016. Hivyo basi, Harakati ya Kujitenga ya Eneo la Kusini inayo ongozwa na Hassan Baoum, aliye patiliza utelekezaji, ni harakati ya kisiasa inayo husishwa na usaidizi wa mwanzoni wa Amerika na kuwa kitovu ambacho kwacho Amerika inaweza kukitumia kuingia Yemen kupitia eneo la Kusini vile vile. Harakati hizi, matukio na mashambulizi haya yalitekelezwa na Al Hirak, na kitovu chake kilikuwa mji wa Dhale. Ingawa Hassan Baoum Hadhrami anatoka Mukalla, na sio Dhale, harakati zote hizi zimehudumu kama vituo vya mafunzo ya kazi ya kisiasa kwa kundi hili. Serikali ya Sana'a mwanzoni haikuiona harakati hii kuwa hatari kwa sababu kazi zake kuu zilikuwa za kisiasa, na hivyo basi, ilikuwa tu ikizikamata nembo zake pekee kama Hassan Baoum, Ahmed bin Farid, Ali al-Gharib na Ali Manasra kwa muda fulani, na kisha kuwaachilia.

3- Hivyo basi, vibaraka wa Amerika katika Harakati ya eneo la Kusini wamepewa ujuzi na kumakinishwa katika wazo la kujitenga, ambayo imekuwa fikra kwao. Huku, wengine waliovutwa na matendo ya Harakati ya eneo la Kusini, inayo chochewa na hisia ya kutelekezwa; baadhi yao ni wanaharakati wa kieneo, na wengine wako chini ya ushawishi wa Uingereza na vibaraka wao nchini Yemen, na mfano wa hawa walikuwa wakati mwengine wakiunga mkono umoja wa nchi na wakati mwengine wakiunga mkono kujitenga kwa nchi, ambapo kujitenga kwa nchi haikuwa fikra yao. Serikali jijini Sana'a ilikuwa ikinufaika na haya kwa kupunguza chachu fikra ya kujitenga kwa nchi ambayo imezungukwa na vibaraka wa Amerika, na ilikuwa ikipenya katika baadhi ya vibaraka wake kwa lengo hilo hilo. Kama tulivyo sema, serikali jijini Sana'a haikuwaona kuwa hatari, lakini ilipo dhihirika kwa serikali ya Raisi Saleh jijini Sana'a na Waingereza nyuma yake kwamba harakati hii inaongeza kasi na kwamba matishio yake yanazidi kuongezeka hususan kwamba vibaraka wa Amerika wako mstari wa mbele katika harakati hii, dola jijini Sana'a, pamoja na Waingereza na wafuasi wao wa kieneo, waliitulizia makini harakati hii ili kuidhibiti, hususan kwa kuwa ilionekana kuwa vigumu kuimaliza huku hisia za kutelekezwa zikikua eneo la Kusini. Mpango "Waingereza" wa kuidhibiti ni kuundwa kwa mujibu wa matukio ya harakati eneo la Kusini, kutokana na majaribio hatari ya kupenya katika kuandama ambayo hayakufungika tu na ukamataji, bali pia kuhusisha ghasia. Hili liliendelea mpaka Imarati ilipo ingia na majeshi yake ya ardhini, kwa kutumia kisingizio cha kuwemo ndani ya muungano wa Waarabu na kisha kushambulia vikali baada ya kufariki kwa Saleh ambapo ushawishi wa Uingereza eneo la Kaskazini ulififia na kuogopea kuwepo kwa pengo endapo Mahouthi watafanikiwa katika kupanua athari yao eneo la Kaskazini. Hivyo basi, ilianza kufikiria kwa makini jinsi ya kuwa na nguvu Kusini itakayo tia shinikizo la kuwepo kwake katika utawala wa Yemen; au hata angaa eneo la Kusini. Kwa hivyo, ilianza kufikiria kwa makini juu ya kumakinisha athari yake eneo la Kusini, hususan kwa kuwa haikuwa ikimtegemea Hadi pekee, kwa kuzingatia kuwa ametawaliwa na Saudi Arabia, hivyo basi ililishughulikia hili kupitia Imarati, pamoja na kuanzisha majeshi ya aliyekuwa Raisi wa Yemen, aliye uawa na Mahouthi mwishoni mwa mwaka jana mnamo 4/12/2017, yaliyoanza kurudi Kusini na kupangwa na majeshi ya Imarati katika kupigana na Mahouthi. "Duru kutoka kwa serikali ya Yemen zimethibitisha kuwa Tarek Saleh, mpwa wa Ali Saleh, alikuwa mjini Aden chini ya hifadhi ya majeshi ya Imarati. Duru za kidiplomasia zimesema kuwa Imarati inatia juhudi kubwa kuondoa vikwazo vilivyo ekewa juu ya Ahmed bin Ali Saleh ili kucheza dori ya kisiasa siku za usoni". (Chanzo: Nass Times, tovuti ya Yemen 5/2/2018), "Tutamuunga mkono Tariq Saleh na tutasimama na yeye katika eneo la Kaskazini na katika maeneo yote mpaka Sana'a itakapo kombolewa kikamilifu", alisema kamanda wa majeshi ya Baraza la Mpito la eneo la Kusini (30/1/2018, France 24). Hii yamaanisha kuwa Uingereza inacheza mchezo eneo la Kusini na kutia nguvu athari yake pamoja na vibaraka wake kutoka kwa jamaa za Ali Saleh wenye ushawishi katika Kikosi cha majeshi ya Kijamhuri ya Yemen na chama cha General Congress. Wanaharakati wa kujitenga walisaidiwa na Imarati, wakijua kuwa Imarati inashiriki kwa majeshi ya angani na ardhini, huku Saudi Arabia ikishiriki kwa majeshi ya angani pekee.

4- Kwa hivyo, Uingereza ilianza kuhudumu eneo la Kusini kupitia Imarati ili kupenya ndani ya Harakati asili ya eneo la Kusini au kuipiga teke kupitia kuunda harakati mpya itakayo ongoza mandhari. Imarati ilianza na mrengo wa Ali Saleh Al-Beidh ingawa Uingereza ilijua uzito wa majaribio ya Amerika ya kumuunga mkono Ali Saleh Al-Beidh na Ali Nasser. Majaribio hayo ya Amerika yanajumuisha kuisaidia Iran, huduma za Misri, kama mkutano wa Harakati ya eneo la Kusini jijini Cairo chini ya uongozi wa Ali Nasser Mohammad mnamo 2014, na huduma za Lebanon, ambapo Beirut imempa Ali Saleh Al-Beidh makao na jukwaa la vyombo vya habari ambavyo alinyimwa na Oman tangu alipo taka hili mnamo 1994. Halafu, kwa kuzuka kwa kimbunga cha Saudia mnamo 2014, alikwenda Riyadh,

*Endelea Uk..14*

ambako alipewa chungu ya pesa. Lakini, kama tulivyo tangulia kusema, Imarati imeanza kuujaribu ushawishi wa mrengo wa Al-beidh na Nasser. Ama kuhusu ni kwa nini imeanza na mrengo huu, ni kwa sababu mbili: Kwanza, kwa sababu anatabanni ghasia, na ya pili ni historia ya utiifu wake kwa Waingereza, kwani walikuwa nyuma ya kuundwa kwa chama chake cha National Front na kuukabidhi utawala wa Yemen Kusini kwake yeye. Kwa hivyo, walimtaka aishi kwa kumbukumbu za enzi hizo, ili wamrudishe kwake au kumkaribisha nao na kuuimarisha. Kufuatia kuanzishwa kwa operesheni za muungano wa Waarabu nchini Yemen mnamo 2015, Al-Beidh alipewa uhamisho kutoka Saudi Arabia hadi Imarati ambako kwa sasa anaishi Abu Dhabi, anaingia katika nchi ambazo ni tiifu kwa Amerika, kwa hivyo ameishi nchini Lebanon kwa takriban miaka miwili (2012 na 2013) akiungwa mkono na Iran na kuhifadhiwa na chama chake huko, kisha kwenda Saudi Arabia na hatimaye kuchukuliwa na Imarati kwa kuwemo kwake ndani ya muungano huo, na kumhamisha kwake kama tulivyo taja awali ambapo anaishi Abu Dhabi na kumzunguka na mazingira ya heshima. Inajulikana kuwa Salem Al-Beidh ni kigeugeu katika utiifu wake; alikuwa mtiifu kwa Waingereza alipo kuwa raisi wa Yemen Kusini na kisha mwanzoni mwa miaka ya tisini alitongozwa na Amerika na kubakia katika utiifu wake huu huku akisafiri katika nchi vibaraka wa Amerika, na sasa yuko Imarati ambayo inajaribu kumtongoza tena, ambapo si ajabu kwake kubadilika tena, na kama itatokea, mambo yaweza kuwa moto baina yake na Imarati. Lakini, msimamo wake uko karibu na Baraza la Mpito na amelisifu: "Aliyekuwa Makamu wa Raisi wa Yemen, Ali Salem Al-Beidh, ametangaza kuunga mkono kwake kuundwa kwa "umbile la kisiasa la eneo la Kusini", siku moja baada ya magavana watatu katika majimbo ya Kusini kumuunga mkono gavana wa Aden, Aideros Zubaidi kuunda umbile hilo. Al-Beidh alithibitisha, katika taarifa iliyo pokewa na gazeti la "Al-Arabi Al-Jadeed", kuwa angeunga mkono mwito huu "kwa njia zozote ziwezekanazo" na kuzisihi nguvu kadha wa kadha za kisiasa eneo la kusini na watu binafsi "kuamiliana kwa uzuri na mwito huu na kujitoa kutoka katika hali ya matarajio, ikhtilafu na kutegemea hatua mpya". Taarifa ya Al-Beidh imekuja siku moja baada ya magavana watatu, gavana Abyan, Khidr al-Saidi, gavana wa Lahi, Nasser Al-Khange, na gavana wa Dhale, Fadl al-Jaadi, kujiunga na mwito huu wa gavana wa Aden, Aidarous al-Zubaidi, wa kuundwa kwa "umbile la eneo la kusini" (16/9/2016). Vile vile, rafikiye, Ali Nasser Mohammed, ambaye wakati mwengine anaunga mkono kujitenga na wakati mwengine anataka serikali moja nchini Yemen lakini kwa masharti ayaonayo yeye! Alipoulizwa kuhusu suluhisho nchini Yemen 4/10/2017 (yaani, kabla ya mashambulizi ya Ali Saleh dhidi ya Mahouthi mwishoni mwa mwaka wa 2017), alisema: "Kuundwa kwa serikali ya umoja wa kitaifa na maafikiano, kuondolewa kwa chembe kuu zinazo sababisha vita pande zote mbili "Mahouthi na serikali ya Hadi" katika vyeo vyovyote rasmi wakati wa kipindi cha mpito na kuondolewa kwa silaha kwa vyama na pande zote na kukabidhiwa Wizara ya Ulinzi kwa kuwa Yemen inahitaji raisi mmoja, serikali moja, waziri mmoja wa ulinzi na kuamua kwenda katika uchaguzi katika hatua ya mbeleni. (Chanzo: Al-Ahram Al-Arabi 4/10/2017). Ni Dhahiri kutokana na haya kuwa Waingereza wamefaulu kupitia Imarati kufikia kiwango cha ushawishi kwa watu na mirengo yao, ambao hawakuichukulia kwa nguvu fikra ya kujitenga ambayo hawatajiondoa kutokana nayo kwa kuwa imetokamana na Harakati ya eneo la Kusini, bali kulingana na dhurufu zinazo wazunguka.

5- Mrengo wa Hassan Baoum kimsingi ulikuwa ni mrengo wa kifikra wa kisiasa wa kujitenga. Waingereza walitambua kuwa masuluhisho yoyote ya kuridhisha, kuvutia au kutawala sio muwafaka, kwa hivyo wakajaribu kumzingira nchini Oman kwa kifungo cha nyumbani kwa staili ya kimatata, pasi na uamuzi rasmi, na alikuwa ashaazimia kwao kwa sababu ulikuwa ukijionesha kutoegemea upande wowote, kana kwamba hakujua kuwa unakwenda sambamba na Waingereza kwa mujibu was dori ulioagizwa kwayo! Kwa hivyo, kupitia vibaraka wake nchini Oman, misumari ilikazanishwa juu ya Hassan Baoum na alikuwa chini ya kifungo cha nyumbani katika mji wa Salalah kwa muda mrefu. Kwa kukosekana huku kwa mtu kinara wa Amerika katika Harakati ya eneo la Kusini, makundi tiifu kwa Amerika katika Harakati hiyo yamedhoofika kwa kiasi fulani. Hivyo basi, Waingereza walichukua fursa ya kupitia Imarati na kuangazia juhudi za kuunda harakati sambamba eneo la kusini ili kuupiku mrengo wa Baoum eneo la Kusini, na kuzima kiu yao kupitia kwa Aidarous al-Zubaidi, ambaye ni kiongozi maarufu katika Harakati ya eneo la Kusini, na mwanzilishi wa Harakati ya kujitenga na kujiamulia wenyewe "HATAM" mnamo 1996. Na kwa ukaribu wake na kundi la Waingereza, aliteuliwa na Raisi Hadi kuwa gavana wa Aden mnamo 7/12/2015, miezi michache baada ya kuanzishwa kwa mashambulizi ya Saudi (Machi 2015). Hii ilikuwa ni ishara yenye nguvu kwa ajili ya kujenga Imani ya vibaraka wa Uingereza kwake yeye. Aidarous al-Zubaidi amezungukwa na mazingira mazito eneo la Aden na alikuwa ni gavana mwenye mafanikio wa mji huo. Aliregesha umeme mjini humo na kuyafurusha magenge ya kisilaha. Alipigana na Mahouthi na kupinga mapendekezo ya mjumbe wa Amerika, Ould Sheikh. Yote hayo ni kwa kupitia usaidizi wa moja kwa moja wa kiraia na wa kifedha na kijeshi kutoka kwa Imarati. Kwa kuwa alikuwa mpiganaji katika vita vya wenyewe kwa wenyewe mnamo 1994 na kiongozi anaye husika na harakati ya kujitenga tangu mwanzoni mwa kuundwa kwake na kufukuzwa na utawala wa serikali ya Ali Saleh jijini Sana'a tangu kuweko kwake mafichoni nchini Djibouti mnamo 1994, na kwa kuwa ni mtoto wa eneo la Dhale, kitovu cha harakati ya eneo la Kusini na nukta ya amali zake, ikiongezewa na mafanikio

*Endelea Uk..15*

yake kama gavana wa Aden na vita vyake dhidi ya Mahouthi, umaarufu wake umeongezeka eneo la Kusini kama mtu mwenye usemi wa kisiasa anaye shindana na uongozi wa jadi wa Hassan Baoum katika Harakati ya eneo la Kusini. Kijeshi, Aidarous al-Zubaidi anamtegemea Hani Ben Breik, mwanzilishi wa Ukanda wa eneo la Kusini, anaye sifiwa pakubwa kuwa mtu wa Imarati eneo la Kusini. Hani Ben Breik, aliye jitokeza katika uwanja wa Yemen kama mpiganaji anaye kabiliana na Mahouthi, na kisha katika mandhari ya kisiasa kama waziri aliye lazimishwa na Imarati kwa nguvu kwa sababu ya ushawishi aliopata kutokana na kusaidiwa kwa ukarimu kutoka Abu Dhabi, na kuanzisha ule unaoitwa "Ukanda wa Usalama", wanamgambo wanasaidiwa hadharani na Imarati eneo la Kusini mwa Yemen. (Chanzo: Sasa Post, 2/11/2017). Kwa hivyo, al-Zubaidi na Breik walikuwa na maslahi eneo la Kusini, lakini kwa sababu walikuwa katika serikali ya Hadi na utiifu wao kwa Uingereza kufichuka hii haitawapatia umaarufu katika kulingania Harakati ya eneo la Kusini, kwa hivyo hatua ya kwanza ilikuwa ni kuwaondoa kutoka katika serikali ya Hadi katika njia itakayo onesha, hususan al-Zubaidi, sintofahamu nzito na kambi ya Hadi na kisha watu wa eneo la Kusini watakusanyika nyuma yao kuunda harakati mpya ya Hirak, na ndivyo ilivyo kuwa.

6- Mnamo Aprili 27, 2017, Raisi wa Yemen alitoa amri ya kutimuliwa kwa Aidarous al-Zubaidi, Gavana wa Aden na Hani Ben Breik, Waziri wa Serikali huku Hani akiagizwa kufanyiwa uchunguzi. Maelfu ya Wayemeni walishiriki katika maandamano katika mji ulioko kusini wa Aden, wakipinga maamuzi ya Hadi, na makundi katika Harakati ya eneo la Kusini yaliotangazwa katika "Tangazo la Aden" mnamo 4 Mei 2017 uamuzi wao wa kumteua Aidarous al-Zubaidi kuunda na kuongoza kundi kusimamia na kuwakilisha Kusini ili kupata malengo na matamanio yake, kuongezea pia na kumpa mamlaka kamili kuchukua hatua zozote muhimu za kutekeleza vipengee vya tangazo hilo. Wiki moja baada ya Harakati ya eneo la Kusini kumpa kazi hiyo al-Zubaidi ya kuunda uongozi wa kisiasa na kusimamia na kuwakilisha Kusini, al-Zubaidi alitangaza uraisi wake kwa Baraza la Mpito eneo la Kusini katika mji wa Aden, mnamo 11 Mei 2017, na kumteua Ben Breik kama naibu wake ikiongezewa na uanachama wa watu 26.

Kutokana na mlango wa kushindana na Baoum, alitoa hotuba huku akiiweka iliyokuwa bendera ya Kusini ubavuni mwake (huku akiwa na bendera ya iliyokuwa dola ya Yemen Kusini, al-Zubaidi alisema, katika hotuba iliyo peperusha na runinga mnamo Alhamisi kuwa chini ya "tangazo la kihistoria la Aden", "uongozi mkuu wa kisiasa wa eneo la Kusini unaoitwa Uraisi wa Baraza la Mpito la eneo la Kusini utakamilisha mipangilio yote ya kubuni asasi za Baraza la Mpito la eneo la Kusini, na usimamizi na uwakilishaji wa eneo la Kusini kindani na kinje" (Chanzo: Shirika la habari la CNN Arabic 11/5/2017).

Hivyo basi, al-Zubaidi na Ben Breik na nyuma yao Imarati (Muingereza) wamekuwa ndio nguvu za kuundwa kwa uongozi eneo zima la Kusini. Magavana wa mikoa wanateuliwa na Raisi wa Yemen; yaani, wao ndio vibaraka wa duara la Uingereza nchini Yemen, na waliosalia katika viongozi wa Baraza la Mpito ni wafuasi wake. Aliweza hata kuwajumuisha baadhi ya watu wa mrengo wa Baoum, mithili ya Ali al-Saadi na Nasser al-Khubji, hata kwa kipindi fulani, hivyo ikiwa ukweli utadhihiri, ima wataondoka au kufurushwa, au yaweza kutumiwa kama njia ya kuwatenga. Hivyo basi, Nasser Al-Khubji chini ya mpango wa "kumtenga" Baoum kutoka katika mandhari amekuwa mfuasi wa mwanzo wa al-Zubaidi!

Huku baraza la mpito linalo ongozwa na Aidarous al-Zubaidi likiwa na udhibiti nusu mjini Aden, umiliki wa nguvu wastani za kijeshi zikiongozwa na Ben Breik katika mikoa mengine ya kusini na hata mjini Marib, mkusanyiko wa magavana wa mikoa pambizoni mwa uongozi wa Aidarous al-Zubaidi, usaidizi kwa waliokuwa wafuasi wa ujamaa wa "Dola ya Kusini", kama vile Ali Salem al-Beidh, aliye tangaza mapema uungaji mkono wake kwa al-Zubaidi, usaidizi wa Tariq al-Fadhli na staili yake ya Kiislamu iliyo ongezea uzito katika msimamo wa kabila lake mjini Abyan, msimamo wa kifedha, kisiasa na kijeshi wa Imarati katika upande wake, kwa yote haya, Uingereza ilimakinisha kadhia ya Harakati ya eneo la Kusini pambizoni mwa kibaraka wake Aidarous al-Zubaidi kwa kiwango kikubwa. Ikiwa dhurufu hizi za kisiasa zitaendelea kuwepo kama zilivyo, hususan uwepo wa uzito wa Imarati katika eneo la Kusini, udhibiti huu utaendelea kuwepo.

7- Amerika imetambua kuchelewa kwake, na kuonyesha kuchukizwa kwake, na kile kinacho ashiria kutoridhika kwa Amerika kwa kuundwa Baraza la Mpito ni upinzani wake kwa mjumbe wake wa kimataifa Ould Cheikh kwa Baraza hilo (mjumbe wa UM nchini Yemen, Ismail Ould Cheikh, aliye tumwa kumtimua gavana wa Aden, Aidarous al-Zubaidi, ujumbe "unaotishia wazi" juu ya historia ya tangazo lake la kuundwa kwa baraza la mpito kwa ajili ya kulitenga eneo la Kusini, kwa mujibu wa duru ya kuaminika. Al-Mashad al-Yemen ilinukuu duru ya kuaminika ikisema kuwa Ould Cheikh alikutana na al-Zubaidi na kutuma ujumbe wazi wa vitisho endapo atasisitiza kulishikilia baraza hilo alilolitangaza, ambalo limepingwa na Raisi wa Yemen, Baraza la Ushirikiano wa Ghuba, kundi la Mahouthi na wengine wengi ndani ya Harakati ya eneo la Kusini. Endapo al-Zubaidi atasisitiza, Umoja wa Mataifa na Baraza la Usalama litamjumuisha miongoni mwa wale wanaozuia mpangilio wa amani nchini Yemen na utekelezaji wa azimio nambari 2216, chini ya sura ya VII, na atachukuliwa kama Mahouthi na Saleh kama "waasi" … (Chanzo: Russia Today 14/5/2017).

*Endelea Uk..16*

Inaonekana kuwa Amerika imerekebisha jambo hili, kwa hivyo ikaisisitiza Oman kumuachilia huru Baoum. Baada ya kuachiliwa kwake, Hassan Baoum alichukua hatua kali dhidi ya Baraza la Mpito, akisaidiwa na Imarati katika mzozo mkubwa uliojitokeza wa Kiamerika nchini Yemen, na inaoneka kuwa harakati zake zilikuwa na usaidizi wazi wa Saudia. Hivyo basi, chini ya macho na uoni wao Bunge la kwanza la Baraza la Harakati ya Mapinduzi, likiongozwa na yeye, lilifanywa mjini Aden 17/8/2017, wafuasi wake mia sita wakishiriki, wakiituhumu Imarati kwa kuikalia Yemen Kusini. Taarifa ya kongamano hilo alisema: "Tunapinga wazi unyanyasaji wa watu wetu wa kusini na uenezaji urongo na kuwaathiri kihisia ili kuvutia uungaji mkono na kisha kupindua matakwa hayo ya watu wa Kusini … Tunathibitisha kuwa kiongozi Hassan Baoum, Raisi wa Baraza Kuu la harakati ya mapinduzi, ndiye kiongozi na nembo ya eneo la Kusini ambayo tunajivunia nayo na kujifakhiri kwayo … Yanayo jiri leo eneo la Kusini ya ushindani wa kifujo baina ya majeshi ya nje, kama Imarati, ambayo imekuwa ni nchi inayo nyakua bandari za eneo la kusini na bidhaa zake, na kudhibiti hatma ya watu wetu na mielekeo yao na kisha inakuja kuwapa kipote cha wafuasi wake kiasi kidogo cha makombo." (Chanzo: Adan Al-Ghad 17/8/2017). Yaani, kundi la Baoum linaonesha uadui wazi kwa Imarati na kuitaka kuondoka nchini Yemen, na kongamano la Baoum kuliita kundi la al-Zubaidi "wafuasi wa Imarati, inayowapatia kiasi kidogo cha makombo".

Ni wakati huo ambapo kongamano la pili la Baoum, lililo fanywa mnamo 11/112017, na ilisemwa katika tangazo la mwisho la kongamano hilo la Baoum la pili la kila mwaka la "Baraza la Harakati ya Mapinduzi", lililofanywa mjini Aden na Al-Arabi Al-Jadeed kupata nakala yake, "Tunatoa wito kwa ule unaoitwa Muungano wa dola za Kiarabu kuweko na mazungumzo ya moja kwa moja na Baraza Kuu la Harakati hiyo baada ya kuondoa majeshi yake yote kutoka eneo letu, na tunathibitisha umakinifu wetu katika mafungamano ya kijamii na ya kidini baina yetu. Baraza hilo linaloongozwa na Baoum liliutaja muungano huo kama "dola vamizi" na kuongeza, "Tunathibitisha haki yetu kamilifu ya kukabiliana na uvamizi kwa njia na mbinu zote za halali na kwa wakati na mahali muwafaka kulingana na maslahi yetu ya kitaifa". Taarifa hii ilisisitiza kuwa majadiliano au suluhisho yoyote itakayo iweka kando kadhia ya eneo la kusini na wawakilishi wake halali hayatafaulu kwa sababu wawakilishi hawa halali ndio walioiongoza harakati hii tangu siku yake ya mwanzo na sio wale walioingizwa kibahati, kwa pesa au kufinyangwa na uvamizi wa kigeni" … (Chanzo Al-Arabi Al-Jadeed 11/11/2017). Taarifa hii, ingawa ilizungumzia kuhusu muungano wa Waarabu, kimsingi ilielekezwa dhidi ya Imarati kwa sababu kongamano hilo lilifanywa chini ya ulinzi wa Saudia!

8- Kwa kutamatisha: baada ya Ali Salem Al-Beidh na Ali Nasser Mohammed kushindwa mnamo 1994 na Ali Saleh kunyakua rasilimali za Yemen Kusini, kutelekezwa kwa watu wa Kusini na kuteswa kwa wanajeshi wengi wa eneo la Kusini … yote haya yame sababisha kuzuka kwa harakati nyingi za upinzani kuanzia wakati huo, zenye kuonekana zaidi ni harakati tatu:
- Harakati ya eneo la Kusini, mrengo wa Ali Salem Al-Beidh usio aminika: wakati mwengine ukiwa na Amerika na vibaraka wake, na wakati mwengine ukiafikiana na Uingereza na vibaraka wake.
- Harakati ya eneo la Kusini, mrengo wa Hassan Baoum unaosaidiwa na Amerika na vibaraka wake, hususan Iran.
- Harakati ya eneo la Kusini, mrengo wa Al-Zubaidi unaosaidiwa na Uingereza na vibaraka wake, hususan Imarati.
- Kama tulivyo taja juu, tumeangazia misimamo yao muhimu juu ya kadhia za sasa za Yemen, na inatia uchungu kuwa kadhia zetu zinaingiliwa na wakoloni makafiri kwa kutumia ala za kutu kutoka kwa wenzetu! Hivyo basi, damu yetu inamwagwa nchini Yemen na kwengineko kwa manufaa ya makafiri kwa kutumia ala za ndani ya eneo. Na watu hawa wamesahau au kujifanya kusahau mambo ambayo lau watayatafakari watalia machozi ya damu kwa yale waliyo yafanya:

Allah, Mwenye nguvu, Mwenye uwezo wa juu, amewaharamisha Waislamu kutokana na kuwategemea makafiri:"**Na wala musiwategemee wale waliodhulumu ukakuguseni Moto. Na wala nyinyi hamuna mlinzi badala ya Allah, kisha wala hamutanusuriwa.**" [Hud: 113].

Na Mtume wa Allah (saw) asema kuhusu kumwaga damu pasi na haki kuwa ni jambo kubwa kwa Allah kuliko kuangamia dunia nzima. Tirmidhi amesimulia kutoka kwa Abdullah bin Amr kwamba Mtume (saw) amesema: "Kuangamia dunia nzima ni sahali mbele ya Allah kuliko kumuua Muislamu mmoja."

Na Ibn Assaker ameisimulia katika Muajam yake na kusema: Hii ni hadith Hasan, sasa vipi basi itamwagwa kwa manufaa ya wakoloni makafiri? Hakika, ni kosa juu ya kosa; "**Itawafika wale walio kosa udhalili na adhabu kali kutoka kwa Allah kwa vile vitimbi walivyo kuwa wakivifanya.**" [Al-A'nam: 124]

Lakini, Yemen, iliyosifiwa na Mtume wa Allah (saw) kuwa biladi ya Iman na hikma haikosi wanaume wenye ikhlasi, ukweli na uaminifu ambao watasimama dhidi ya wale wanao watii wakoloni makafiri. Watairudisha Yemen, kwa idhini ya Allah, kuwa Dar Islam, chini ya kivuli cha bendera ya Uislamu, chini ya Khilafah Rashida itakayo regesha hadhi yake kuwa kama Mtume (saw) alivyo isifu katika hadith iliyo simuliwa na Bukhari katika Sahih yake kutoka kwa Abu Hurayrah (ra) kutoka kwa Mtume (saw): " **Watu wa Yemen wamewajia na ni watulivu na wepesi mioyoni. Iman ni Yemen na Busara ni Yemen…**"

**8 Jumada II 1439 H**
**24/02/2018 M**


Email: info@uqab.or.ke